JINA …… KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY, S. L. P. 41 NGORONGORO

KUMB.NA.ESS/F.I/JOINING/2021/01 MOB NO. 0767-446188(HEADMASTER)

MOB NO. 0766-086309 (SECONDMASTER)

MOB NO. 0756-681629(MALEZI)

Ndg…….. TAREHE 18/12/2020

S. L. P. ……

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY MWAKA 2021.

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Embarway ipo umbali wa km. 283 kusini kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro (Loliondo). Usafiri wa basi kutoka mji wa Loliondo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Loliondo nauli ni Tsh 23,000/=

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 24/01/2021.
Ni matarajio yetu kuwa mwanafunzi ataripoti kwa wakati ili asipitwe na masomo

Asante na karibu sana Embarway Sekondari

……. HEADMASTER EMBARWAY SECONDARY SCHOOL P. O. Box 41 NGORONGORO

BONIFACE B. SAMIDAI
MKUU WA SHULE

1:1 SARE

Wavulana/ wasichana

i. Suruali 2 –za kijani cha shule grade one. Mwanafunzi atakayeshonewa suruali za kubana(mnyonyo) hatapokelewa.
ii. Sketi 2–za kijani cha shule grade oneyenye rinda boksi (box) na urefu usiopungua sentimita 10 toka goti. Mwanafunzi atakayeshonewa sketi fupi hatapokelewa.
iii. T–shirt 2 zenye nembo ya shule kwa gharama ya 9000@ zipo shuleni
iv. Shati 2 nyeupe yenye mikono mifupi kwa wasichana na wavulana
v. Sweta 2kijani wasichana na wavulana
vi. Viatu vyeusi vyangozi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu jozi 2
vii. Soksi nyeupe jozi 2 kwa wasichana na nyeusi jozi 2 kwa wavulana
viii. Tai 02 za kijanizenye mistari nyeupe kwa wavulana na wasichana

Nguo za kushindia: (shamba dress)

i. Suruali/ sketi 2 za kaki ya polisi mashono kama sare za shule
ii. Kanga pea 1 au kitenge pea 1 kwa wasichana
iii. Taulo kwa wavulana na wasichana

Nguo za michezo

i. Tracksuit 01yenye nembo ya shule utaikuta shuleni kwa Tsh 30,000/=
ii. Raba nyeupe jozi 1 kwa wasichana na rangi yoyote kwa wavulana na bukta ya Njano Jozi 1 kwa wasichana na wavulana

Vifaa vya bweni

i. Shuka (bed sheet) 2 Bluu Bahari kwa wavulana na pink kwa wasichana
ii. Godoro ya inchi 3 futi $2^1/_2$ kwa futi 6
iii. Neti ya mbu 3ft x 6ft
iv. Blanketi 1 rangi yoyote
v. Tranker 1 ya bati ngumu

NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi.

Vifaa vya taaluma.

i. Madaftari 10 quire 3
ii. Dictationary /kamusi– oxford English to English
iii. Begi la kubebea madaftari (liwe madhubuti) la mgongoni
iv. Kalamu za wino 10, pensili na rula
v. mathematical set 01
vi. Karatasi za matumizi ya mwanafunzi (Ream 1)
vii. Faili la kutunzia mitihani

Vifaa vya usafi: (kwa mujibu wa waraka na 6 wa mwaka 2015)

i. Fekeo (slasher) 1. Kwa wasichana na panga kwa wavulana
ii. Fagio ngumu (hard broom) 01 na rubber squizer 01na fagio ya chelewa 01
iii. Toilet paper 5 sabuni za kufulia miche 03 au zaidi na kuogea za kutosha
iv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko,visiwe vya plastic
v. Ndoo 01 ya kuogea lita 10

Matibabu

1. Kwa mujibu wa waraka wa elimu Na 6 wa mwaka 2015 kila mzazi atatakiwa kugharamikia matibabu ya mtoto wake. Hivyo hakikisha mwanao anakuja naBima yake ya afya kwa mwenye nayo. Shule inatoa huduma ya kwanza tu. Iwapo mwanafunzi atapelekwa hospitalini kwa matibabu zaidi mzazi atagharamia.
2. Hakikisha mwanao amepimwa na taarifa zake zijazwe kwenye fomu iliyoambatanishwa hapo nyuma. Asipopimwa hatapokelewa.

SHERIA ZA SHULE: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu msingi nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi. Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
3. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa na wazazi ni muhimu.
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
5. Kuheshimu wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, wimbo wa shule, picha za viongozi ni lazima.
6. Kuzingatia usafi wa mwili na mazingira ya shule ni sharti na siyo hiari.
7. Kuzingatia ratiba ya shule na kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa kuwa hivyo
8. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea maeneo yafuatayo kwa sababu zozote zile
    a) Vilabu vya pombe
    b) Majumba ya starehe kama night clubs, pubs, kasino n.k
    c) Nyumba za kufikia za wageni.
    d) Kutembelea nyumba za watumishi
9. MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA SIMU SHULENI.

MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI AONDOLEWE SHULENI MARA MOJA.

- Wizi
- Ulevi wa aina yeyote
- Uvutaji sigara , bangi na madawa ya kulevya
- Kupigana au kupiga
- Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
- Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
- Kuoa au kuolewa
- Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- Kukataa au kugoma adhabu kwa makusudi
- Uasherati, ubakaji na ushoga
- Kuacha shule kwa siku 90 mfululizo utakuwa umejifukuzisha shule mwenyewe
- Kumiliki na kutumia simu ya mkononi.

JINA ……KIDATO CHA KWANZA 2021

SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY

FOMU YA KUIKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA (I) 2021

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza kisha iletwe shuleni siku ya kuripoti (ithibitishwe na Mwenyekiti/Afisa Mtendaji wa kijiji wa eneo unaloishi)

Mimi …… kwa hiari yangu ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha kwanza 2021 katika shule ya sekondari embarway. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria za shule kama ilivyoandikwa kwenye ukurasa wa 3 kwa wakati na nitastahili aidha kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kusimamishwa masomo. Endapo nitatenda makosa yaliyoainishwa, kisheria ni vema hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kunifukuzisha shule mara moja kabla sijaleta athari kubwa kwa shule kinidhamu na kitaaluma.

Tarehe …….. …….

Sahihi ya mwanafunzi

Mimi …… mzazi/mlezi wa …….

Nakubali/ sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote alioko shuleni analazimika kufuata sheria za shule kama ilivyoainishwa hapo juu na kuwa mtiifu kwa walimu ambao ndio walezi wake.

- Nitahakikisha kuwa mtoto wangu atakuwa shule kwa kipindi chote cha masomo, na endapo atashindwa kuja shule kwa sababu zozote nitatoa taarifa kwa walimu mapema. Nimeelewa kuwa akiacha shule kwa siku 90 mfululizo kama sheria ya wizara husika inavyosema atakuwa amejifukuzisha shule.

- Nitahudhuria vikao vyote vya wazazi shuleni na kufuatilia kwa ukaribu maendeleo ya mwanagu kinidhamu na kitaaluma.

……. Tarehe ……

Sahihi ya mzazi/mlezi

Mimi …….. ninathibitisha kuwa ndugu …….. ni mzazi/ mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kuingia kidato cha 1 Embarway sekondari 2021.

…….. tarehe ……

Sahihi ya mwenyekiti wa mtaa/kijiji

Muhimu: Kurasa zote kuanzia 1 hadi ukurasa wa 7 lazima kurudishwa ofisini zikiwa zimejazwa vizuri na kutiwa saini na wahusika wote kwani ndiyo fomu zitakazofungua jalada la mwanafunzi.

JINA …….KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Mimi …….. nimesoma sheria za shule na taratibu zote naahidi kuzitekeleza kwa uaminifu mkubwa na kufuata ushauri wa walimu.

Nitahudhuria masomo yote kila siku; na kufanya mazoezi, majaribio yote na mitihani yote kikamilifu. Sitashiriki katika hila zozote za wizi au udanganyifu wa mitihani, nitashiriki katika klabu za kimasomo na michezo mbalimbali shuleni na wala sitaacha shule kamwe bila taarifa.

Nitahudhuria maandalio (preparation) yote ya mchana na usiku ili kujisomea na si kwingine. Nifukuzwe shule maramoja endapo nitaonekana nazurura mitaani, porini (wakati wowote) bwenini wakati wa vipindi au kujisomea siku za masomo, au siku za jumamosi na jumapili (week-ends).

Ninaahidi kusoma kwa bidii na kuwatumia walimu wangu vizuri kitaaluma na nitatii mashauri yote yanayotolewa na wazazi/walezi na walimu wangu siku zote.

Michezo ninayoshiriki vizuri

1. ……
2. ……
3. ……

Naweza kushiriki vema katika fani za ndani.

1. Kwaya ( )
2. Ngoma ( )
3. Maigizo ( )
4. Ngonjera ( )
5. Muziki ( )

Weka (√) kubainisha unavyoweza kushiriki.

Nitashiriki kikamilifu katika kazi zote za mikono, natambua kuwa migomo na vurugu ni haramu hivyo sitashiriki wala kushawishi wengine kujihusisha.

Nitawasilisha matokeo ya mitihani na majaribio pamoja na barua nitakazopewa shuleni kwa mzazi/mlezi wangu.

JINA LA MWANAFUNZI……

SAHIHI ……

TAREHE ……

HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……..(majina matatu)
2. Tarehe ya kuzaliwa ……..(kama ilivyo kwenye cheti)
3. Dini …… dhehebu ……..
4. Mahali na wilaya alipozaliwa …….
5. Shule ya msingi alikohitimu darasa la saba……..
6. Kazi yeyote ya uongozi alizowahi kushika akiwa shuleni

Madaraka/uongozi	Shule mahali	Mwaka

7. Mambo anayopendelea kufanya nje ya masomo
   a) ……
   b) ……..
   c) …….

HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la baba……..(majina matatu)
2. Kazi yake ……dini ……..
3. Jina kamili la mama ……(majina matatu)
4. Kazi yake …….. dini ……
5. Anwani na namba ya simu ya mzazi onyesha ni baba au mama
   …….baba/mama
   ……

   Simu ……..(baba)…….(mama)
6. Nyumbani (mahali anapoishi baba/mama wa mtoto
   Wilaya …….. kijiji……kata……..
7. Jina la M/kiti wa mtaa……..
8. Jina kamili la mlezi…… Iwapo mtoto haishi na wazazi wake
9. Anwani kamili ya mlezi ……. Simu……
10. Dhehebu atokalo mzazi ambalo mtoto wake atalelewa……..
11. Anwani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakwenda siku za likizo
    ……
    …….
12. Ndugu wa mwanafunzi watakao kuja kumtembelea mwanao

	JINA	UHUSIANO
i.	.....	……
ii.	…….	……
iii.	.....	……
iv.	…….	……
v.	……	……

Mimi ……baba/mama/mlezi wa ……nathibitisha kuwa taarifa hizo hapo juusahihi na ninaahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba mwanangu anakuwa na tabia nzuri, mwenye bidii ya masomo na asiyezurura mitaani nyakati za masomo na hata siku za weekend.

PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NGORONGORO DISTRICT EMBARWAY SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM 2021

To be completed by **Medical officer only**

Name of student ……..Age…….

1. HIV test ……
2. Blood count (White & red)……
3. Urine examination ……
4. UTP……(For female)
5. Stool examination ……
6. Syphilis test ……
7. TB test ……
8. Ear test ……
9. Eye test ……
10. Abdomen ……
11. Spleen ……
12. Additional information or any other physical, mental hereditary or infections diseases
    ……..
    (please state nature of treatment)

Medical certificate

I certify that the above mentioned student has been examined and found him/her to be fit/unfit to pursue further education.(delete whichever not needed)

Name …… signature ……
Designation …… station ……
Date ……

Official stamp

NB fomu hii lazima ijazwe na Daktari katika Hospitali inayotambulika na serikali kamwe isipelekwe kwenye vituo vya afya vya watu binafsi.